# Turudia Biblia

**1997**

# MASOMO

| Somo: | Ukarasa: |
|---|---|
| 1. Kwa Nini Tuirudie Biblia? Boaz Kasiba | 03 |
| 2. Je, Biblia Ni Kitabu Chenye Mamlaka Ya Kuongoza Kanisa? Boaz Kasiba | 05 |
| 3. Imani Katika Kristo. Peter Kamatula | 07 |
| 4. Toba Na Kukiri. Lazima Newton | 08 |
| 5. Mpango Wa Wokovu. Linkosi Mkwama | 09 |
| 6. Hatua Zinazotuelekeza Wokovuni. Linkosi Mkwama | 12 |
| 7. Maisha Ya Ukristo. Lazima Newton | 14 |
| 8. Kanisa. Bernard Kulanga | 15 |
| 9. Ndimi Au Lugha. Robert Stapleton | 17 |
| 10. Miujiza #1. Robert Stapleton | 19 |
| 11. Miujiza #2. Robert Stapleton | 20 |
| 12. Kazi Za Wanawake. Joshua Mwakyasima | 21 |
| 13. Ibada Ya Sabato. Robert Stapleton | 22 |

## Kwa Nini Tuirudie Biblia

**Utangulizi:**

Vitabu vya watu ni vya watu, viumbe ni wenye kufanya makosa wanaotengeneza na kuhubiri mafundisho yenye makosa.

**Mwili:**

I. Kwa nini tuirudie Biblia?
- A. Inadaiwa kuwa ni Neno la Mungu, Ebr. 1:1, 2; 2:2-4; 2 Tim. 3:15-17; 2 Pet. 1:20-21.

II. Sasa hivi Mungu anaongea kupitia kwenye Biblia.
- A. Anaongea kupitia kwa mwanawe, 2 Tim. 3:15.
- B. Inatwambia kwamba Mungu anajieleza kwetu kama mwenye uwezo, "kiumbe," asiyeshindwa au anguka, Mtawala na Mwokozi.
- C. Tunajua kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu.

III. Biblia ni neno la Mungu ilitolewa kwetu kwa kupitia kwa Mwanae kwa njia ya Roho Mtakatifu.
- A. Tuunganike pamoja naye 1 Yn. 1:6-7.
- B. Yaliyoandikwa katika neno ndiyo yatakayoamua nani atakayechukuliwa na Yesu kwenda kwa Baba yake, I Kor. 15:24, 28; Ebr. 12:2.
- C. Neno lilitolewa kupitia kwenye mnyororo wa amri, Mungu-Yesu-Roho Mtakatifu-waandishi waliovuviwa. Yn. 14:26; 16:13; 15:26-27.
    1. Ilitolewa kwa miujiza, Mk. 16:19-20; Ebr. 2:3-4.
- D. Aliyofundisha Yesu aliyoyaleta na kuyatuma yote yalikuwa kweli:
    1. Imani katika Kristo-Mdo. 24:24
    2. Imani ya injili-Fil. 1:27
    3. Imani -Mdo. 16:15.
    4. Ukombozi wa milele-Yuda.
    5. Injili ya milele-Ufu. 14:6
    6. Kufunuliwa yaliyokuwa hayajulikani -Efe. 3:3-5.
- E. Kweli sasa ni Biblia, Mt. 15:9
    1. Biblia imetufanya tuwe wakristo, Yak. 1:18; I Pet. 1:22-23; Rum. 1:16; 1 Kor. 15:1-2.
    2. Pia tutahukumiwa kwa Biblia, Yn. 12:48; Rum. 2:16; Ufu. 20:12.

**Hitimisho:**

1. Katika vitabu vyote duniani leo, ni kimoja pekee kisemacho kuwa ni cha Mungu kupitia kwa Mwanae na kuongelea ya mbinguni. Na kuongeza ni kwamba Biblia haijichanganyi yenyewe.

2. Hivyo kama kipo kitabu ambacho tunapaswa kukifuata ni Biblia, I Pet. 1:3-4.

## Je, Biblia Ni Kitabu Chenye Mamlaka Ya Kuongoza Kanisa?

**Utangulizi:**

1. Watu wengi huamini kwamba kwa vile tu wanafuata nyayo za watu wema wa dini basi wataokolewa, Mt. 15:9; 1 Kor. 2:5.
2. Binadamu anahitaji kiongozi; Biblia ndio kiongozi:
    - A. II Pet. 1:21
    - B. I Pet. 4:11
    - C. II Tim. 3:16-17
3. Mungu ametoa kiongozi wa kufuatwa kwa muda wa vipindi vyote.

**Mwili:**

I. Kipindi cha Wazee au cha Mababu.
- A. Katika historia ya kipindi cha kwanza cha Biblia Mungu aliongea na Mababa, Ebr. 1:1.
- B. Je, Mungu alikuwa na mpango au ushirika nao?
    1. Mwa. 6:5-aliona udhaifu ni mkubwa.
    2. Mwa. 6:3-akaamua kuwateketeza wote.
    3. Kuanzia msitari wa 14 katika sura ya sita tunaona ushirika.
        - a. Nuhu akaufuata huo mwongozo-Mwa. 2:22.
- C. Mungu alikuwa na mwongozo kwa mababu?
    1. 1 Pet. 3:20.

II. Kipindi cha Musa:
- A. Kipindi cha pili katika historia ya Mungu zilitolewa sheria kupitia kwa Musa, Yn. 1:17.
- B. Zilitolewa katika Mlima Sinai, Kutoka 19:1.
    1. Wakapewa Amri Kumi, Kut. 19:20.
    2. Je, Kulikuwapo na mwongozo katika kipindi cha Musa?
- C. Mungu akatoa Amri Kumi ambazo zilikuwa msingi wa Sheria za Musa kwa ajili ya Waisraeli tu, Kut. 34:27.
    1. Walipewa mwongozo, Kut. 34:27.
        - a. Kwa muda wote wa Sanduku la Agano, Kut. 25-27.
    2. Walipewa sheria ziwe mwongozo katika ibada zao na maisha yao pia.
        - a. Kut. 20:4; Kut. 32:1-14; Kut. 32:8; Kut. 32:20-28.

III. Kipindi cha Ukristo:
- A. Miaka 900 baada ya Musa kupokea sheria za zamani, Yeremia aliongea kuhusu Agano Jipya, Yer. 31:31-34.
- B. Agano Jipya lingekuwa tofauti na la Musa.
    1. Sheria zingeandikwa katika mioyo sio kwenye jiwe, Ebr. 8:10.
    2. Zingekuwa kwa watu wote wala sio waisraeli tu, Mt. 28:18-20.
    3. Kutokana na sheria hizi watu wangesamehewa dhambi zao na

zisingekum bukwa tena Mdo. 2:38; 22:16; Ebr. 10:1-14.

C. Kipindi cha Ukristo kilianza mara baada ya kufa, kuzikwa na kufufuliwa kwa Kristo, Ebr. 8:6-13; 9:17.

D. Je, Tunao mwongozo?

1. Ni nini, ni wapi, na ni nani kiongozi ambaye mamlaka yatoka kwake?
    - a. Msikilizeni Yeye-Mt. 17:1-5
        - 1) Kol. 2:14.
    - b. Yesu alisema; mamlaka yote nimepewa mimi, Mt. 28:18
        - 1) Yn. 12:48; Mt. 24:35
        - 2) 2 Yn. 9-11.
    - c. Kuna kiongozi wa Kanisa:
        - 1) Agano Jipya ni kiongozi ili uwe Mkristo.
            - a) Kusikia-Rum. 10:17.
            - b) Kuamini-Yn.8:24.
            - c) Kutubu-Lk. 13:3.
            - d) Kukiri-Rum. 10:10.
            - e) Kubatizwa-Mdo. 2:38.

**Hitimisho:**

Mwongozo wa Mungu katika Agano Jipya ni kwamba wote watakaoamini, kutubu na kumkiri Kristo na wakabatizwa katika Kristo watakuwa wakristo. Hivyo ili Wakristo waishi maisha ya imani ni lazima wafuate mwongozo wa Agano Jipya.

## Imani Katika Kristo

Dibaji:

1. Wanadamu tunapaswa kuwa na imani ili tuweze kuupata wokovu, Yn. 3:16; Efe. 2:8.
2. Tusipokuwa na imani Mungu hawezi kupendezwa nasi, Ebr. 11:6.

Mwili:

I. Maana ya imani, Ebr. 11:1
- a. Imani inapatikana kwa kusikia neno la Kristo, Rum.10:17.
- b. Yesu alisema mtu hawezi kumwendea yeye mpaka avutwe na Baba yake, Yn. 6:44.
- c. Kinachomvuta mtu ili amwendee Yesu ni neno la Mungu, Yn. 6:45.
- d. Imani katika Kristo inapatikana baada ya mtu kuyasikia maneno ya Kristo mwenyewe, Yn. 12:48.

II. Kule kusema "imani ni kuwa na hakika ya mambo yasiyoonekana" haina maana kuwa mambo hayo tuliyaona awali, la!
- a. Tunapaswa kuamini kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu japokuwa hatujawahi kumwona.
  1. Tunaamini Yesu aliishi duniani na alitufia wenye dhambi kwa kusoma Biblia, 1 Kor. 15:1-4; Mdo. 15:7.
  2. Tuchunguze maandiko, Mdo. 17:11, 12.

III. Imani iletayo wokovu ni ile iliyo katika Kristo, Mdo. 16:31.
- a. Imani iambatane na kumkiri Kristo .
  1. Wayahudi walimwamini lakini hawakumkiri, hivyo hawakupata wokovu, Yn. 12:42, 43.
  2. Tusipomkiri Yesu naye hatatukiri mbele za Mungu, Mt. 10:32, 33.
- b. Imani iwe na matendo, Yak. 2:17, 19, 24.
- c. Imani iwe n matumaini ya kufika mbinguni.
  1. Yesu ni njia, Yn. 14:6.

IV. Katika imani tunapaswa kutii sheria ya injili.
- a. Tufanye aliyotuamuru Yesu ili tudumu katika imani ya kweli, Lk. 6:46.
- b. Mtu alisiyeitii injili hana sababu ya kumwita Kristo "Bwana, Bwana," Mt. 7:21.
- c. Imani iwe na upendano wa ndugu, 1 Pet. 1:22.

Mwisho:
1. Imani katika Kristo iambatane na sheria zote za Yesu zilizoamriwa katika injili.
2. Tunapaswa kuzingatia sana upendo katika imani, Mt. 22:37, 39.
   - a. Tumpende Mungu.
   - b. Tupendane sisi kwa sisi.

## Toba Na Kukiri

Toba ni nini?

Toba kwa ufupi wa kueleweka ni “mgeuko” yaani mgeuko wa yale uliyokuwa unayafanya na kisha kuacha, Mdo. 9:35.

I. Kutubu kwa maana ya makosa, Mdo. 8:22.
- a. Kurudi, Isa. 7:3; Hes. 22:34.
- b. Kuhuzunika, I Kor. 7:9-10.

II. Kwa nini ugeuke na kurudi?
- a. Kwa sababu hujui muda, Mt. 25:13.
- b. Kwa sababu ya kutambua kosa, Zab. 51:10-13.
- c. Kwa sababu ya kutambua wokovu, 2 Pet. 3:9, 15.
- d. Kwa sababu ya kutambua wapatikana sasa, 2 Kor. 6:2; Ebr. 3:15-19.

III. Mifano ya watu waliotubu agano la kale.
- a. Akani, Yosh. 7:20-22.
- b. Mfalme Sauli, 1 Sam. 15:24.
- c. Farao, Kut. 9:27; 10:16.
- d. Ezra, Ezr. 9:6-7.

IV. Mifano ya watu waliotubu Agano Jipya.
- a. Petro, Lk. 5:4-11.
- b. Mwana mpotevu, Lk. 15:18
- c. Siku ya Pentekoste, Mdo. 2:37-39, 40-41.
- d. Towashi, Mdo 8:34-37.
- e. Kornelio, Mdo 10:1-6, 44-47.
- f. Lidia na mlinzi wa gereza, Mdo. 16:13-31.

Mwisho:

Tumeona I-IV sisi nasi tu binadamu kama wao ni sharti tukiri kwa midomo yetu, Mt. 10:32-33; Rum. 10:9-10, tuendelee kumkiri Yesu katika maisha yetu, 1 Pet. 4:16 na kuwa waaminifu hadi kufa, Ufu. 2:10; 3:11-12.

**Mpango Wa Wokovu.**

Sikia

Amini

Tubu

Kiri

Batizwa

Biblia inafundisha kwamba dhambi ni uasi wa sheria ya Mungu, 1 Yn. 3:4. Watu wote wanaojua tofauati ya jema na baya, wametenda dhambi, Rum 3:23. Dhambi zetu hututenganisha na Mungu, Isa. 59:1, 2. Adhabu ya dhambi ni kifo, Rum. 6:23. Hii ndiyo mauti ya pili, ambayo ni ziwa la moto, Ufu. 21:8.

Mungu atupenda. Hapendi tuadhibiwe kwa ajili ya dhambi zetu. Kwa hiyo, ametoa njia ya kusamehewa, Yoh. 3:16, Mungu alimtuma Mwana wake wa pekee, Yesu Kristo, kufa kwa ajili ya dhambi zetu. I Yoh. 4:10, Yesu alipata mateso tuliostahili sisi kupata kwa ajili ya dhambi zetu. Isa. 53:4-6, hakufa kwa sababu ya dhambi zake mwenyewe, yeye hakufanya dhambi hata moja. II Kor. 5:21, aliteseka kwa ajili ya dhambi zetu juu ya msalaba ili tuweze kusamehewa, Rum. 5:6-8; I Pet. 2:24.

Ili tuweze kusamehewa dhambi zetu, tuweze kupokea uzima wa milele, tunapaswa kuupokea wokovu alioufanya Kristo tayari. Kuna hatua tano unazopaswa kuzifanya ili kupata wokovu huo.

<u>1. Sikia habari njema ya Yesu Kristo.</u>

Jambo la kwanza tunapaswa kusikia habari njema ya Yesu Kristo. Biblia inafundisha kwamba imani chanzo chake ni kusikia na kusika huja kwa neno la Kristo, Rum. 10:17. Mtu hawezi kuwa mkristo kwa sababu ya imani ya wazazi wake. Haiwezekani kurithi imani, Eze. 18:20. Kila mtu binafsi anapaswa kumwamini Yesu Kristo mwenyewe. Ukristo ni dini ya kufundishwa, Mat. 28:19-20. Kabla mtu hajajifunza Biblia na kufahamu kwamba Yesu Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zake. Alizikwa na kufufuka kutoka wafu. Hawezi kuokolewa, I Kor. 15:1-4. Mtume Paulo aliandika akisema watamwiteje wasiyemwamini na watamwaminije wasiyemsikia, na watamsikiaje, pasipo mhubiri, Rum. 10:14? Kwanza mtu anapaswa kusikia habari njema kabla ya kuamini.

<u>II. Amini kuwa Yesu ndiye Kristo Mwana wa Mungu:</u>

Jambo la pili, mtu anapaswa kuamini kwamba Yesu ndiye Kristo Mwana wa Mungu aliye hai, Mt. 16:16. Yesu alisema mtakufa katika dhambi zetu msiposadiki ya kuwa mimi ndiye, mtakufa katika dhambi zenu, Yoh. 8:24. Mlinzi wa gereza kule Filipi, aliwauliza

Paulo na Sila, yanipasa nifanye nini nipate kuokoka? Walimwambia mwamini Bwana Yesu nawe utaokoka pamoja na nyumba yako, Mdo. 16:30-31. Yesu alisema pia aaminiye na kubatizwa ataokoka asiyeamini atahukumiwa, Mk. 16:16. Mtu hufikia kumwamini Yesu Kristo baada ya kusikia injili ikihubiriwa, imani chanzo chake ni kusikia na kusikia huja kwa neno la Kristo, Rum. 10:17. Hii ndiyo sababu kwamba injili inapaswa kuhubiriwa sana, Mk. 16:15.

## III. Tubu dhambi.

Jambo la tatu; mtu anapaswa kutubu dhambi zake akitaka kuokolewa, Mdo. 17:30, 31. Yesu aliagiza kwamba, toba na ondoleo la dhambi lihubiriwe katika jina lake kwa mataifa yote, kuanzia yerusalemu, Lk. 24:47. Toba ni matokeo ya kujuta kwa sababu ya dhambi zako, II Kor. 7:10. Wayahudi kwenye Siku ya Pentekoste baada ya kugundua kwamba walikuwa wamemsulubisha Mwana wa Mungu walichomwa mioyoni mwao, Mdo. 2:37. Walitaka wasamehewe dhambi zao, kwa hiyo waliuliza tutendeje ndugu zetu? Waliambiwa tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi, Mdo. 2:37-38. Mtu anapotubu, hugeuka kutoka dhambini, I Thes. 1:9. Anaonyesha kwamba, ametubu kwa kuanza kufanya matendo mazuri, Mt. 3:8.

## IV. Kukiri kwamba Yesu ndiye Kristo.

Jambo la nne, mtu anapaswa kukiri kwamba Yesu ndiye Kristo Mwana wa Mungu aliye hai, Mt. 16:16. Ukweli mkuu huu ndiyo msingi kulikojengwa Kanisa la Kristo, Mt. 16:18; Mdo. 4:11, 12; I Kor. 3:11. Yesu alisema kwamba tunapaswa kumkiri mbele ya watu, ikiwa tutahitaji naye atukiri mbele ya Baba yake, Mt. 10:32, 33.

Mtume Paulo aliandika: lakini yanenaje? Lile neno li karibu nawe, katika kinywa chako na katika moyo wako; yaani, ni lile neno la imani tulihubirilo. Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa mtu hukiri hata kupata wokovu, Rum. 10:8-10.

Filipo alipomhubiria Towashi habari za Yesu, Towashi aliuliza swali, ni nini kinachonizuia nisibatizwe? Filipo akasema, "Ukiamini kwa moyo wako wote itawezekana. Akajibu akanena, naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu," Mdo. 8:35-38. Tunapaswa kufanya ukiri muhimu huu na rahisi ili tuweze kuokolewa.

## V. Batizwa toswa majini.

Jambo la tano, mtu anapaswa kubatizwa ili aweze kuokolewa. Yesu alisema aaminiye na kubatizwa ataokoka, Mk. 16:16. Tafadhali zingatia kwamba ubatizo hufuata kuamini. Mtu asiyeamini katika injili hawezi kubatizwa kiukweli. Kwa hiyo watoto wachanga hawawezi:

1. Kuwa na dhambi

2. Kusikia injili
3. Kutubu dhambi
4. Kukiri kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu aliye hai. Ubatizo pia unafuata toba, Siku ya Pentekoste, Petro aliwaelezea wale waliouliza cha kufanya ili waokolewe tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi, Mdo. 2:39. Mtu hawezi kubatizwa kiukweli ikiwa hajatubu kiukweli.

Ubatizo ni maziko katika maji, Rum. 6:3, 4; Kol. 2:12. Kwa hiyo kunyunyiza na kumwaga maji kichwani si ubatizo sahihi. Ubatizo ni kwa kusudi la kuokolewa, Mk. 16:16; 1 Pet. 3:21. Mtu haokolewi kabla hajabatizwa (kutoswa) ubatizo ni kwa ajili ya ondoleo la dhambi, Mdo. 2:38. Kama vile Yesu alivyo mwaga damu yake kwa ondoleo la dhambi, Mt. 26:28. Kwa hiyo tunabatizwa kwa kusudi la kupata ondoleo la dhambi katika ubatizo dhambi za mwenye dhambi husafishwa kwa damu ya Yesu, Mdo. 22:16; Ufu. 1:15.

Mtu anatakiwa afanye nini akitaka kusamehewa dhambi zake? Anapaswa.

1. Kuisikia injili ya Yesu Kristo, Mt. 17:5; Rum. 10:17.
2. Kuamini kwamba Yesu Kristo Mwana wa Mungu
3. Kutubu dhambi zake zilizopita.
4. Kukiri kwamba Yesu ndiye Mwana wa Mungu.
5. Na kubatizwa kwa ondoleo la dhambi. Ukifanya hivyo, bwana atakuzidisha kwenye kanisa lake, mdo. 2:41,47. Utakuwa umezaliwa mara ya pili, Yn. 3:3-5; 2 Kor. 5:17. Utakuwa ndani ya Kristo ambamo kuna baraka zote za rohoni, Efe. 1:3; Gal. 3:26, 27. Kwa ufupi yeye ni mkristo, Mdo. 11:26; 26:28; 1 Pet. 4:16.

Je, Wewe umeokolewa kutoka dhambini? Je, Umezifuata hatua za wokovu hizi rahisi? Kama hujafanya hivyo, basi fanya hivyo leo.

**Hatua Zinazotuelekeza Wokovuni**

Hali ya wanadamu ya kutisha katika dhambi ingelikuwa mbaya kabisa kama isingekuwa ni upendo mkuu wa mungu alionao kwa ajili ya wanadamu.

Kwa hiyo ukweli ni kwamba upendo wa mungu ulimpasa afanye mpango wa kuwaokoa wanadamu toka katika utumwa wa dhambi, Kut. 3:7-8; Yn. 3:16; Mpango huo ni injili, Rum. 1:16. Injili ni uweza wa mungu uletao wokovu, kwa sababu inaelezea ukweli kuhusu Yesu Kristo kuwa ni Mwana wa pekee wa Mungu na mwokozi wa ulimwengu.

Kusudi kubwa la injili ya Kristo ni upendo waajabu wa mungu kwa ajili ya wanadamu aliounyesha kwa kumtoa Yesu Kristo msalabani Kalvari, umekuwa wokovu kwa ajili ya watu wote, Yn. 3:16; Rum. 5:8-9.

Lakini tunapaswa kutambua kuwa kufa kwa Yesu Kristo msalabani kungelikuwa batili kama asingelifufuka, I Kor. 15:14, 20; Rum. 4:25. Kwa sababu hiyo uweza wa injili unaleta wokovu.

Sasa na tutafakari mambo tofauti katika injili yanayo wahusu wanadamu wanavyoweza kuepukana na dhambi kwa njia ya Bwana na Mwokozi Yesu Kristo.

1. <u>Wokovu</u>: katika dhambi wanadamu wamepotea: Kwa hiyo wanahitaji kuponywa au kuokolewa. Yesu ndiye wa kwanza kuwaokoa watu katika dhambi. Na wokovu unapatikana ndani ya Yesu tu, Mdo. 4:12; Mt. 1:21. Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja kufatufa na kuokoa kile kilicho potea, Lk. 19:10; Ebr. 2:9-10; 7:25; 1 Tim. 1:15; Rum. 8:1.

2. <u>Ukombozi</u>: (Fidia-rudisha haki). Mwenye dhambi yupo katika utumwa wa dhambi na Shetani, Rum. 6:16. Gharama iliyolipwa kwa ukombozi ni damu ya thamani ya Yesu iliyomwagika msalabani. Ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani msamaha wa dhambi, Kol. 1:14; Mdo. 20:28; 1 Kor. 1:30; 6:20; Ebr. 9:12. Katika kumkomboa mwanadamu kutoka katika utumwa huo wa dhambi, Yesu aliondoa kabisa uwezo na kazi za Ibilisi.

3. <u>Utakaso</u>: (Kusamehewa) ikiwa mtu ameokolewa na kukombolewa kwa uweza wa damu ya Kristo, anahesabiwa kama mtu mwenye haki, mnyofu, mtu anayekubaliwa mbele za Mungu, Rum. 3:24; Mdo. 13:38-39; Rum. 5:1; Tito. 3:7.

4. <u>Upatanisho</u>: Neno hili linafafanuliwa kama "Kurejeza tena urafiki baada ya mtengano," mtu anapotenda dhambi yake ya kwanza, anatengana na Mungu. Lakini anapokuwa ameokolewa amekombolewa, na kuhesabiwa haki katika Kristo, hupatana na Mungu, anaurudia upendeleo wa Mungu, Kol. 1:21-22. Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupa tanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo, naye ametia ndani yetu neno la upatanisho, 2 kor. 5:18, 19; Efe. 2:16-17.

5. Msamaha: Ili tusimame mbele za Mungu bila udhuru, wanadamu wanapaswa kuwa wamesamehewa dhambi zao, ikiwa na maana kwamba lazima wawe wametubu makosa waliyomkosea mwenyezi Mungu. Makosa mtu yanapokuwa yamesamehewa huwa yameondolewa ama yamefutwa kabisa, kana kwamba hajawahi kutenda. Ni kwa njia ya damu yake Kristo ndipo Mungu anapotusamehe makosa yote aliyotendewa.

Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, msamaha ya dhambi, sawa sawa na wingi wa neema yake, Efe. 1:7; Mdo. 5:31; 13:38; 26:18; Efe. 4:32; Kol. 1:14; 3:13; 1 Yoh. 1:9; 2:12. Neno lenye maana sawa na "msamaha" ni "ondoleo la dhambi," soma Mt. 26:28; Lk. 1:17; Ebr. 9:22.

6. Usafi: dhambi huifanya roho ya wanadamu kkuwa chafu kama vile mavumbi na masizi yanavyochafua mwili wa mwanadamu. Kama vile tunavyotumia maji kuondoa uchafu wa mwili kadhalika tunapotoswa katika Kristo tunapata damu ya Bwana Yesu Kristo, hivyo ndivyo roho inavyosafishwa na uchafu wa dhambi. Huyo alikuja kwa ushuhuda, ili aishuhudie ile nuru wote wapate kuamini kwa yeye, Yoh. 1:7; 1 Kor. 6:11; Ufu. 7:14; Rum. 6:1-6.

Kuziinua juu nguvu za Yesu Kristo na damu yake ya kuokoa, kukomboa, kutakasa, kupatanisha, kusamehe na kusafisha ni kuiinua juu neema ya Mungu, kwa sababu yote Yesu anayowafanyia wenye dhambi inaonyesha neema ya Mungu, ambayo bila ya hiyo hakuna anayeweza kukombolewa kutoka dhambini. "Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda; hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu," Efe. 2:4-7; Mdo. 20:32; Rum; 3:4; Tit. 2:11; 3:7; Ebr. 2:9.

Neno "neema" lina maana ya wema anaopewa mtu ambaye hastahili kupewa; katika maneno mengine ni upendeleo asiostahili. Hakuna anayestahili utakaso na wokovu; hakika anachostahili ni kupoteza nafsi yake katika jehanamu ya milele, Rum. 1:32. Kwa hiyo, mtu anapopokea wokovu kwa njia ya dhabihu ya Yesu Kristo, ikiwa amekombolewa na damu yake ya thamani atapata kile ambacho anastahili, Efe. 2:7; Rum. 6:23.

Yesu Kristo ndiye tumaini la ulimwengu:
Ikiwa tunatamani kutoka katika dhambi zetu na kwenda katika ufalme wa milele wa Mungu tunapaswa kuwa na uhakika kwamba tumekuja kwa Mungu kwa njia ya Kristo na damu yake, Yn. 14:6.

Lakini endapo tutakataa wokovu mkuu huu tutapoteza roho zetu jehanamu ya milele. Kwa hiyo imetupasa kuyaangalia zaidi hayo yaliyosikiwa tusije tukayakosa.

Kwa maana ikiwa lile neno lililonenwa na malaika lilikuwa imara na kila kosa na uasi ulipata ujira wa haki, sisi je! Tutapataje kupona, tusipojali wokovu mkuu namna hii? Ebr. 2:1, 3.

## Maisha ya Ukristo

Maisha ya ukristo ni ya kusaidia wengine kufundisha, Fil. 4:3; Kol. 1:23; 1 Pet. 2:2; 2 Pet. 3:18; Efe. 1:18; 4:15.

I. Maisha ya ukristo kwanza ni:
- a. Kujitoa kwa hiari, Mk. 14:36; Rum. 12:1-2.
- b. Kujitoa kwa kupenda, Mt. 22:37; 1 Tim. 3:1.

II. Maisha ya ukristo ni sharti uelewe unachofundisha:
- a. Kutoka Biblia, Isaya 54:13; Yoh. 6:45; Neh. 8:8; Mt. 11:28-30.
- b. Angalia, chunguza kisha thibitisha, Mit. 14:15, 1 Thes. 5:21; Mhu. 8:5.
- c. Fuata ukweli mtupu, Yoh. 17:17; 8:32.
- d. Kisha fundisha, Mt. 28:19; 2 Tim. 2:2.
    - 1. Fundisha bila kinyume, Mt. 16:13-17; Mt. 15:8-9.

III. Maisha ya ukristo ni sharti:
- a. Kuwa kielelezo, 1 Tim. 4:11-12
    - 1. Kufundisha
    - 2. Usemi, 1 Kor. 15:33
    - 3. Mwenendo
    - 4. Upendo
    - 5. Imani
    - 6. Usafi.

IV. Maisha ya ukristo sharti yawe ni ya:
- a. Kukua, 2 Pet. 1:5-11
- b. Kutoa kwa moyo si kwa unafiki, Mt. 6:1-4; 1 Kor. 9:6-8.
- c. Kukusanyika kila Siku ya Kwanza yajuma kuabudu, Ebr. 10:25.

V. Maisha ya ukristo ni ya kuiga mfano wa:
- a. Yesu Kristo, Lk. 19:10; Yoh. 17:18; Mt. 20:28.
- b. Wenzetu wa awali, Mdo. 8:4; 13:49-15:7.

Mwisho:

Tumeona hayo, na tujiulize sisi mmoja mmoja tulipo, mwenzetu Paulo anasema Efe. 4:13.

## Kanisa

Sehemu ya Kwanza

Maana ya Kanisa:

1. Biblia haitaji kanisa kuwa: Ukatoliki, Uprotestanti au Uyahudi. Si madhehebu fulani wala jumuia ya madhehebu fulani.

2. Neno la asili lenye maana ya kanisa ni la Kiyunani "Ekklesia". Na maana yake ni walioitwa. Angalia: Kol. 1:13; Ebr. 5:8, 9; Mk. 16:16; Mdo. 2:47.

3. Neno hilo hutajwa kwa maana ya ujumla (Mt. 16:18). Na kwa maana isiyo ya ujumla (Rum. 16:16).

4. Kupata maana dhahiri ya kanisa:
   a. Mwili wa Kristo, Efe.5:23; 4:4; Kol. 1:18.
   b. Nyumba (Familia ya Mungu - 1 Tim. 3:15; Gal. 3:26, 27; Efe. 1:3.
   c. Ufalme wa Mungu - Ufu. 17:14; Mdo. 8:12; Mt. 16:18, 19.
   d. Shamba la mizabibu la Bwana - Yn. 15:1-8

Sehemu ya Pili

Lilivyokuja:

1. Lilikuwa katika mawazo ya Mungu kabla ya misingi ya dunia (Efe. 1:3-6).
2. Unabii wa kuja kwake (Isa. 2:2, 3; Yoe. 2:28, 29; Dan. 2:44).
3. Kulikuwa na ahadi ya kanisa (Mt. 3:2; 16:18; Mk. 9:1; Lk. 24:46-49); kisha mdo. 2.

Sehemu ya Tatu

Uanzishwaji wake:

1. Mdo. 2:1-6.
2. Mdo. 2: 12-17, 21.
3. Mdo. 2:32-41, 47.
4. Hivyo, Kristo alianzisha kanisa Yerusalemu, mwaka 33 B.K. na limekuwepo tangu hapo mpaka atakaporudi tena.

Sehemu ya Nne

Kitambulisho chake:

Kuna alama au vigezo vingi vionyeshwavyo na Biblia kuhusu kanisa lililosahihi:

1. Alianzisha nani, Mt. 16:18.

2. Lilianza wapi, Lk. 24:45-49.
3. Lilianza lini, Mdo. 2 - Siku ya Pentekoste.
4. Linaitwaje, Rum. 16:16; 1 Kor. 12:27.
5. Wafuasi waitwaje, Mdo. 11:26.
6. Nani kiongozi, Kol. 1:18.
7. Mangapi, Efe. 4:4.
8. Taratibu zake za mtu kuingia:
    a. Imani (Ebr. 11:6).
    b. Toba (Mdo. 17:30).
    c. Kukiri (Rum. 10:9, 10).
    d. Ubatizo (Mk. 16:16, Mdo. 2:47).
9. Taratibu zake za ibada:
    a. Kukutanika siku ya kwanza ya juma, Mdo. 20:7.
        1) Sala, mdo. 2:42.
        2) Neno, 2 Tim. 2:15.
        3) Chakula cha Bwana, 1 Kor. 11.
        4) Kutoa, I Kor. 16:2.
10. Mafundisho: Biblia, Ufu. 22:18, 19; Gal. 1:6-11.
11. Muundo wake:
    a. Kiongozi, (Kristo Efe. 5:23)
    b. Viongozi wa makusanyiko (yakijitegemea -wazee na mashemasi - 1 Tim. 3; Tito. 1).

12. Ujumbe wa wahudumu:
    a. Kuhubiri injili, Mk. 16:15, 16.
    b. Kusaidia wahitaji, Gal. 6; Yak. 2.
    c. Kuwajenga washiriki, Ebr. 3:12-14.

13. Kila mkristo kuishi maisha ya uaminifu:
    a. Kutoipenda dunia, 1 Yoh. 2:15; Yak. 4:4.
    b. Kuzaa matunda ya roho, Gal. 5:22, 23.
    c. Kudumu katika imani, Ufu. 2:10.

Mwisho:
Mtu atakaye wokovu atajihoji kwa moyo wa uaminifu ili aone biblia (kwa urahisi tu) inasema kanisa ni nini (kama muhtasari huu ulivyokumbusha), kwa nini lilikuja na vipi (kama muhatasari huu ulivyokumbusha) na linajipambanua kwa kitambulisho gani (kama baadhi ya alama zilivyoorodheshwa); kisha atachagua kuingia katika kanisa halali la Mungu, kwa mujibu wa Biblia.

Mungu akubariki ulijue kanisa lake. Amina

## Ndimi au Lugha

Utangulizi:

1. Biblia inatumia neno ulimi katika njia tatu.
    a. Kiungo cha mwili, Yak. 3:5
    b. Kihusika katika kuongea, Mith. 28:23; Yak. 3:6
    c. Ni lugha ya kuwasiliana kupeana mawazo, Dan. 1:4; Mdo. 1:19; 26:14.

2. Harakati za wanadini wa kipentekoste wanadai magawanyiko mawili ya zawadi za ndimi.
    a. "Ndimi" nyingine-zinasemekana kuwa lugha za kigeni za mwanzo zinazozungum zwa kama ushuhuda wa kupokea Roho Mtakatifu ubatizo na kuupata wokovu, Mdo. 2:4.
    b. "Ndimi zisizojulikana" zisemwazo kuwa lugha za mbinguni au kuongea mfululizo kunakosemwa na baadhi ya waliookoka kujionyesha wenyewe kuwa wameiva, 1 Kor. 14:2.

3. Kuna maneno matatu ya kuangalia sisi wenyewe katika somo hili:
    a. Alama-Mk. 16:15-20
    b. Aina-katika neno hili tunaimarishe iwapo lugha zilikuwa kweli ni lugha zinazoeleweka au ni kuongea tu mfululizo.
    c. Maana-katika neno hili tunakusudia kuona jinsi mtu alivyopokea zawadi ya ndimi.

Muundo:

I. Vipi kuhusu lugha zilizosemwa katika Agano Jipya?
    a. Mfano wa kwanza wa kunena kwa lugha lilikuwa matendo 2, baada ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, Mdo. 1:25-2:4, 7, 14.
        1. Kunena kwa lugha ilikuwa alama kwa umati walio pata ujumbe wa wokovu ambao ulihubiriwa siku ile.
    b. Mfano wa pili ulikuwa katika Mdo. 10 ambapo nyumba ya wamataifa ilifanya hivyo kwa njia ya Roho Mtakatifu.
        1. Kama zawadi kama katika Mdo. 2 ni wazi ilikuwa katika lugha inayoeleweka.
        2. Zawadi hiyo hapo ilikuwa alama-Mdo. 11:18, kwamba mataifa wamepewa injili.
    c. Mfano wa tatu ilikuwa katika Mdo. 19 ambapo Waefeso walifanya hivyo kwa kuwekewa mikono na mitume, mbaada ya kubatizwa - Mdo. 19:5-6.
        1. Neno la Kigiriki "glossia" limetumika katika hali zote tatu.
        2. Kwa vile mifano yote hii ya kwanza ilikuwa na lugha kamili kuliko katika mfano wa tatu ndimi ni lazima zilikuwa ni lugha kamili.
    d. Mfano wa nne ulikuwa katika 1 Kor. 14 ambapo Wakorintho walikemewa kwa kukataa zawadi ya lugha.

1. Tukubaliane kuliweka neno lugha kama lilivyo katika Kitabu cha Matendo.
    a) Kwa vile katika matukio yote matatu katika matendo yalikuwa ni lugha kamili 2, 10, 19 naye Paulo akaenda Korintho katika sura ya 18 kwa nini wale watu wapokee kitu tofauti?
2. Wapentekoste wanatueleza kuwa Wakorintho waliongea jambo tofauti kuwa ni lugha zisizojulikana.
3. Paulo na mwenzake wamethibitisha kuwa zile zilikuwa ni lugha kamili kwa kutoa hoja kubwa mbili.
    a) Hoja ya kwanza inaongelea lugha katika dunia, 1 Kor. 14:10-11.
    b) Hoja ya pili inalinganisha "lugha nyingine katika Agano la Kale" na Siku ya Pentekoste, 1 Kor. 14:21, Isa. 28:11-13; Mdo. 2:4.
4. Paulo pia anataja lugha kuwa zilikuwa ishara kwa wasioamini sio wanaoamini, 1 Kor. 14:22

II. Vipi kuhusu kunena kwa lugha siku hizi?

a. Kwa kukubaliana na kwa uaminifu zinatuambia kwamba kwa vyo vyote ambavyo kunena kwa lugha kulikuwa katika Agano Jipya, kulikuwa na kunapaswa kuwa vile vile siku hizi.
    1. Kama kunena kwa lugha kuna nafasi siku hizi, maana ya kupokea zawadi ingekuwapo.
        a) Kubatizwa kwa Roho Mtakatifu kulikoma.
            1) Hakuna ripoti ya kubatizwa kwa Roho Mtakatifu baada ya Matendo 10; Efeso 4:5.
        b) Mitume wote wamekwisha kufa hiyo inamaanisha kuwa hiyo haipo tena.
    2. Kama kunena kwa lugha kuna nafasi siku hizi basi ingekuwa ni lugha kamili (inayoeleweka) siyo mambo yasiyoeleweka.
    3. Kama kunena kwa kugha kungekuwapo leo ingekuwa ni ishara kwa kueneza ujumbe wa injili kwa ajili ya wokovu.

b. Suluhisho la haki ni kwamba mwujiza wa kunena kwa lugha umekwisha, 1 Kor. 13:8.

Suluhisho:

1. Kama kunena kwa lugha kupo siku hizi, basi sheria ya 1 Kor. 14 ingetumika, 1 Kor. 14:13, 22, 26, 27, 28.
    a. Sheria hizo zimedharauliwa na Wapentekoste.
2. Kinachoitwa kunena kwa lugha siku hizi ni upuuzi wa mambo ya kisaikolojia-ambayo ni mlipuko wa ndani wa mtu kwa mafundisho fulani na hali ya mazingira-watu wenye kutamani kupata nafasi ya kiroho.

## Miujiza

Utangulizi:

1. Wako watu wengi ambao wanadai kufanya miujiza kama alivyofanya Kristo na wanafunzi wake.

2. Lakini tunachotaka kuangalia siku hizi:
   - a. Shabaha mahususi ya miujiza.
   - b. Kuonyesha tofauti kati ya rekodi ya miujiza katika Agano la Kale na kile kiitwacho miujiza siku hizi.

Muundo:

I. Shabaha ya miujiza katika vipindi vyote ilikuwa ni kueneza neno la Mungu.

II. Kuna tofauti kubwa kati ya miujiza iliyorekodiwa katika Agano Jipya iliyotolewa na watu waliopewa nguvu ya roho na kile kiitwacho miujizaa siku hizi.
   - a. Angalia mifano ifuatayo:
      1. Mathayo 9:18-22
      2. Matendo 3:1-10
      3. Matendo 9:32-35
      4. Matendo 28:1-6

III. Mapendekezo mengine kulingana na madai yanayotolewa siku hizi.

**Miujiza #2**
**Kukoma Kwa Miujiza**

Utangulizi:

1. Swali sio kama ni kweli miujiza iliyotajwa katika Biblia ilitokea kweli.
    a. Wote tunaamini na kufundisha ilitokea.
2. Maswali ni kwamba ilikuwa ya ujumla au kwa kusudi malumu?
    a. Likuwa ya muda au ya kuendelea?
3. Kwamba karama hizi zingekokma ni dhahiri kwa ukweli ufuatao:

Jambo Lenyewe:

I. Likuwa ni ahadi na kamwe si kwa sala au msingi wa matendo, Yoe. 2:28-32; Mt. 3:11,12; Yn. 14:16,26; 16:7-15; Lk. 24:49; Mdo. 1:5.

II. Ni nani waliohusishwa katika ahadi hizo?
    a. Yoeli 2:28-32.
    b. Mt. 3:11, 12.
    c. Mk. 16:17, 18.
    d. Mdo. 2:38, 39.

III. Angalia, yoeli alitaja muda maalum wa kutimilika.
    a. Siku za mwisho, Isa. 2:1-4; Mik. 3:9-12; 4:1-2.

IV. Angalia sehemu nyingine mbili zinazohusu somo hilo hilo.
    a. Efeso. 4:5.
    b. 1 Kor. 13:8-12.

V. Angalia makusudi yake yalikuwaje na yalivyotimilizwa.
    a. Kipimo cha ubatizo wa Roho Mtakatifu kwa mitume kilikuwa na kusudi lenye pande tatu:
        1. Kufunuia injili
        2. Karama za roho ziweze kutendeka bayana.
        3. Kulithibitisha neno (ujumbe).
    b. Mambo yalitimilizwa nyakati za mitume.
        1. Haja hiyo haipo leo

Mwisho:

1. Kwa ushuhuda huo mbele yetu tunahitaji kuhitimisha kwamba wakati huu hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu na karama maalum leo.

## Kazi Za Wanawake

Utangulizi:

1. Kwa nini adamu aliumbwa?
2. Kwa nini hawa aliumbwa?

I. Somo: usawa wa mwanaume na mwanamke.
  a. Tangu mwanzo mwanaume na mwanamke ni sawa.
  b. Wanao wajibu tofauti tofauti kati yao.

II. Mifano ya wanawake katika Agano la Kale.
  a. Yokebedi-mama yake Musa, Hes. 26:59
  b. Esta-alihatarisha maisha yake kuokoa Israeli.
  c. Debora-aliwafaya Israeli wawe na amani miaka 40.

III. Mifano ya wanawake katika Agano Jipya.
  a. Prisila-alimsaidia mmewe kuwafundisha watu, Mdo. 18:26.
  b. Dorkasi-alijaa matendo mema, Mdo. 9:36.
  c. Lidia-alisababisha nyumba yake iokolewe, Mdo 16:14.
  d. Eunike na Loisi walimfundisha kijana Timotheo, 2 Tim. 1:2.

IV. Nafasi ya wanawake.
  a. Wanawake walikuwa washiriki sawa na wanaume katika kanisa lilipoanza, Mdo. 8:12; 16:14-15; 17:4, 12.
  b. Wanawake ni viungo katika kanisa, 1 Kor. 12:12-30; Gal. 3:27-28; Mdo. 2:47.

V. Wajibu wa wanawake leo. Ni ule ule haubadiliki.
  a. Tito. 2:5-wanawake wazee wafundishe wanawake vijana.
  b. 2 Tim. 1:5-7 - Wanawake wafundishe watoto, 2 Tim. 3:15.
  c. Kuabudu pamoja na wanaume, 1 Kor. 12:12-30.

VI. Jamii na jumuia zao hubadilika lakini sio neno la Mungu, Ebr. 13:8; 2 Yn. 1:9.

VII. Wanaume na wanawake lazima wafuate utaratibu wa Mungu juu yao, 2 Tim. 3:16-17; Gal. 1:6-9; 1 Tim. 2:8-13; 1 Kor. 14:34.

Hitimisho:

Ufu. 22:18-19; 2 Yoh. 9.

## Ibada ya Sabato

Utangulizi:

1. Neno sabato lina maana ya pumzika.
    - a. Biblia inaiongelea ama inatokana na siku ya saba ya juma la Kiyahudi.
    - b. Ilisherehekewa kama siku takatifu, Kut. 20:10.

Muundo:

I. Kuitunza au kuishika sabato kulianza lini:
- a. Maelezo ya kwanza ya kuishika sabato yapo katika Kut. 16:22-30
    - 1. Yanaonyesha kwamba hawakuwa wameuzoea huo utaratibu.
- b. Sheria ya sabato walipewa wayahudi wa zamani tu, Kut. 20:1-2; 34:27-28.
    - 1. Hawakuwa wamepewa baba zao, Kumb. 5:1-13
    - 2. Hawakupewa mataifa, Kumb. 4:8; Rum. 2:14.
- c. Sabato ilitolewa lini, Neh. 9:13, 14.

II. Kwa nini sabato ilitolewa?
- a. Ni ishara kati ya Mungu na Israeli, Kut. 31:16, 17.
- b. Kukumbuka utumwa wa Misri, Kumb. 5:12-15.

III. Mambo zaidi kuhusu sabato kuishika sabato hakutufungi sisi.
- a. Sabato-ambayo ni sehemu ya Amri Kumi iliondolewa na 2 Kor. 3:7-11.
- b. Mitume hawakuwahi kufundisha kuishika sabato:
    - 1. Walifundisha kukusanyika siku ya kwanza ya juma, Mdo. 20:7; 1 Kor. 16:1-2.

<u>Baadhi ya Malengo ya Kuangalia.</u>

A. Sabato ya milele, Kut. 31:16
- 1. Milele kwa maana ya kwamba kadiri ya yale yaliyokuwa chini ya hukumu yalikuwa na nguvu mpaka yaondolewa.
- 2. Hivyo kwa vile sheria ilikuwa bado ina nguvu ilikuwa ni lazima kuishika sabato.

B. Yesu aliishika sabato:
- 1. Pia aliishika Pasaka, Je! Sisi?